Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) Muhtasari

Rakesh Rajani na George Omondi

HakiElimu: Mfululizo wa Mada za Uchambuzi Namba. 2003. 6S

Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) Muhtasari[1]

Rakesh Rajani na George Omondi[2]

Utangulizi

Serikali ya Tanzania imetambua umuhimu wa kuwekeza kwa watu wake kwa nia ya kupambana na magonjwa, umaskini na ujinga. Tangu mwaka 1995, kumekuwa na mfululizo wa mageuzi kushughulikia tatizo linalokwamisha elimu. Hali ya miundo mbinu haijafanyiwa marekebisho na kumekuwepo na upungufu wa mahitaji muhimu. Wanafunzi wengi wanasoma ndani ya madarasa yaliyojaa na yenye upungufu wa madawati, wanafunzi ishirini hata zaidi wanalazimika kuchangia kitabu kimoja. Walimu hawalipwi vizuri na hawajaandaliwa vyema kwa usimamizi na ubora wa majukumu wanayoyafanya. Kanuni za ufundishaji darasani na mahusiano ya mwalimu na mwanafunzi ni ya kiburi na ukatili badala ya kuwa ya kuheshimiana na kujaliana. Umaskini uliokithiri na madeni umekwamisha uwezo wa Serikali kutoa rasilimali husika katika elimu na kutoa uwezo wa kaya kuendana na ongezeko la gharama za elimu. Changamoto nyingine ni UKIMWI ambao umepunguza uwezo wa wananchi na kubebesha mzigo mkubwa unaoongeza umaskini na kuzidisha kutoendelea.

Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) 2002-2006 (URT 2001a) una mkakati wa kupambana na tatizo hili. Unakusudia kutoa nafasi kwa watanzania wote kupata elimu bora kama nyenzo ya Tanzania kupambana na umaskini. Elimu ni sekta iliyopewa kipaumbele na inachukuliwa kuwa ni 'kiini cha maendeleo' katika sera ya kuondoa umaskini (PRS, URT 2000). Sambamba na dira ya 2025, elimu inayosisitizwa si yoyote ile. Bali ni:

> *"Elimu ichukuliwe kama mkakati kwa kuweka mageuzi ya kifikra na kuunda taifa lililoelimika vizuri, lenye maarifa ya kutosha yanayohitajika katika kutatua kwa ufanisi na kiushindani changamoto ya maendeleo inayoikabili nchi. Kutokana na hilo, mfumo wa elimu hauna budi kupangwa upya na kubadilishwa kwa ubora unaolenga katika kukuza ubunifu na utatuzi wa matatizo." (Dira 2025 ukurasa 19, kama ilivyonukuliwa na URT 2001a)*

Nguzo za "upatikanaji, usawa na ubora kwa watoto wote" ndiyo misingi ya MMEM (ukurasa 2). Inaendana na makubaliano ya Tanzania katika mikataba ya kimataifa kuhusu Haki ya Mtoto na Elimu kwa Wote. Muhimu zaidi ni kuwa MMEM imetilia mkazo masuala ya utawala; hasa katika mfumo wa uboreshaji wa mabaraza ya ngazi za chini, kama ilivyo katika mageuzi ya Serikali za Mitaa (URT 1998). Msisitizo uko katika uwazi, demokrasia, ushiriki katika maamuzi na uwajibikaji. Vilevile MMEM inasisitizia lengo la Serikali kujenga mtazamo wa sekta pana zaidi, kwa maana ya kuwa juhudi yote ya Serikali juu ya elimu ya msingi na misaada ya wafadhili inaandaliwa kupitia MMEM badala ya kuwa na mitazamo tofauti ambayo haitaleta maendeleo sawia na yenye gharama kuiendesha.

---

[1] Muhtasari huu umeandaliwa kusaidia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi kufahamika kwa upana zaidi kwa wanaojishughulisha na maswala ya maendeleo, watetezi, wahamasishaji na umma kwa ujumla.Tunaamini utachangia katika kuibua mijadala kuhusu mwelekeo wa elimu ya msingi na mafanikio yaliyopatikana mpaka sasa, kwa sababu mijadala ya namna hiyo ni muhimu kwa demokrasia na maendeleo. Mada hii ya Uchambuzi ilichapishwa kwa mara ya mwanza na HakiElimu katika lugha ya Kiingereza mwaka 2003

[2] Rakesh Rajani ni Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu. George Omondi ni mwanafunzi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Misingi Mikuu ya MMEM

Watu wengi wanafikiri MMEM inahusu ujenzi wa madarasa na kuandikisha wanafunzi tu. MMEM ina nguzo kuu nne: kuongeza uandikishaji, kuinua ubora wa elimu, kujenga uwezo na kuboresha nyenzo za kifedha na watu pamoja na kuzibadili taasisi. MMEM inatambua wazi kuwa mambo yote manne ni muhimu na yanaingiliana na budi yafanikishwe kwa pamoja.

1. Upanuzi wa Kuandikisha

MMEM inakusudia watoto wote wenye kati ya miaka 7 – 12 wawe wameandikishwa darasa la kwanza kufikia Septemba 1, 2004. Idadi ya wanaoandikishwa kila mwaka inatazamiwa kuongezeka kwa asilimia 50 kufikia milioni 1.6 kwa kila mwaka kati ya 2004 hadi 2006, kabla ya kudhibitiwa tena kufikia wastani wa milioni moja (angalia jedwali). Hii itawawezesha watoto wote waliokwama nje ya shule kupata elimu rasmi, hata hivyo baadhi ya wachache walio na umri mkubwa watapatiwa elimu maalum. Mbinu kuu zitakazotumika kuongeza uandikishaji ni kama ifuatavyo:

- *Kuondoa ada*: "Kuondoa ada na michango mingine ya lazima kuanzia Januari 2002 ili kusiwe na mtoto anayenyimwa elimu" (ukurasa 5).

- *Kuajiri na kuwapa motisha walimu*: "Kuajiri, kutoa mafunzo na kusambaza walimu wa kutosha wa shule za msingi kwa namna ambayo itatosheleza ongezeko kubwa la uandikishaji" na "kuhakikisha kunakuwepo na mgawanyo sawa na wenye uwiano wa kijinsia wa walimu waliopata mafunzo" (ukurasa 6). Marupurupu yatolewe kwa walimu wanaofanya kazi katika maeneo magumu kuhakikisha wapo wa kutosha. Kuwapatia nyumba na ajira inayokidhi mahitaji ndiyo mikakati muhimu.

- *Kujenga madarasa na nyumba za walimu*: "Kujenga madarasa mengine mapya" (pamoja na vyoo na maji), " kuwapatia nyumba walimu kama kivutio cha usambazwaji kwa kutoa kipaumbele kwa walimu wa kike katika maeneo yaliyo mbali sana na yale ya vijijini" na "kuwapatia nyumba asilimia 30 ya walimu wapya kwa mwaka" (Ukurasa 7).

Jedwali: Malengo ya Uandikishaji ya MMEM 2002-2006 (kurasa 5-7)

Mwaka	Nafasi Darasa la 1	Walimu waajiriwa wapya	Ujenzi wa madarasa mapya
2002	1,500,000	9,047	13,868
2003	1,600,000	11,651	13,396
2004	1,640,969	10,563	14,203
2005	1,041,880	7,286	6,794
2006	1,065,843	7,249	5,832
Jumla	**6,848,692**	**45,796**	**54,093**

2. Kuinua Ubora

MMEM inakusudia kufufua na kuboresha elimu ya msingi, kwa kuangalia sehemu tatu muhimu: a) kuboresha mbinu na njia za walimu za ufundishaji b) kuhakikisha upatikanaji wa vifaa bora vya kufundishia na kujifunzia, na c) kuhakikisha ubora unadhibitiwa (ukurasa 9). Kimsingi sehemu hizi ni:

- *Kuongeza uwezo na mbinu za walimu darasani*: Walimu watasaidiwa kuweza kufundisha kwa namna ya usomi na umahiri, inayowapa mazingira mazuri watoto na kuzingatia jinsia" (ukurasa 9) na kutumia njia zinazozingatia ujenzi wa ujuzi wa kudumu, tukizingatia ugonjwa wa UKIMWI (ukurasa 10). Kiasi cha dola 40 (takriban shilingi 40,000/=) kitatengwa kwa kila mwalimu kila mwaka, kwa maendeleo na mafunzo (ukurasa 10).

- *Kuongeza vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika ngazi ya shule:* MMEM itatengeneza "mazingira ya shule yanayofaa kwa kujifunzia" (ukurasa 11). Kila mwanafunzi, kufika mwaka 2006, atakuwa na kitabu chake cha kiada. Muhimu zaidi "ili kuanzisha pato la uhakika kwa matumizi mengine ya lazima nje ya mshahara, ruzuku ya uendeshaji ya dola 10 (takriban shilingi 10,000/-) kwa kila mwanafunzi aliyeandikishwa itaanzishwa nchi nzima kuanzia Januari, 2002" (ukurasa 11). Kwa kuanzia dola 4 zitapelekwa kwenye halmashauri za wilaya "kwa ununuzi wa vitabu na vifaa vyingine vya elimu" (ukurasa 11), baadae hizi nazo zitapelekwa moja kwa moja mashuleni, kulingana na mfumo wa uboreshaji wa Serikali za Mitaa ruzuku ya uendeshaji itapelekwa mashuleni ambao "wataamua njia bora ya kuzitumia" (Ukurasa 11).

- *Kuwawezesha viongozi kuwasaidia walimu*: "Viongozi wa elimu (wakaguzi, wakufunzi, walimu wakuu n.k.) watapewa mafunzo ya kuwawezesha kutoa msaada ufaao kwa walimu, badala ya mtindo wa kutoa amri na maelekezo (ukurasa 9).

3. Kujenga Uwezo

MMEM ina lengo la kujenga uwezo na umahiri wa watumishi wa ngazi zote, kwa ajili ya kufanikisha ubora, kugawa madaraka, ushiriki wa umma na kuwezesha jamii. Programu ina sehemu nne:

- *Kufundisha na kuwapa motisha walimu*: Mitaala ya ufundishaji walimu itaangaliwa upya kuona kama inakidhi mbinu za ufundishaji. Serikali itatoa mafunzo kwa kundi kubwa la walimu wapya, wanaokisiwa kufikia 46,000 katika kipindi cha miaka mitano ya MMEM. Maslahi mazuri ya kazi na vigezo vya utoaji huduma vitatolewa kwa walimu "vikwazo vya kifedha kutatuliwa kwa walimu watakaoajiriwa" (ukurasa 12).

- *Kujenga uwezo wa usimamizi wa shule*: Mafunzo ya usimamizi yatatolewa kwa walimu wakuu, kamati za shule, maofisa elimu wa kata na watumishi wengine ili kuongeza ubora, uwajibikaji, ufanisi na kufanikisha ushiriki wa jamii, uwiano wa jinsia na uwezo wa kupambana na athari za VVU/UKIMWI. Kufanikisha haya "watumishi na wadau wote" wanaosimamia MMEM watapatiwa "taarifa za msingi na miongozo juu ya MMEM" pamoja na mafunzo ya utendaji (ukurasa 13). Msisitizo mkubwa uko kwenye kamati za shule, ambazo zitapewa mafunzo juu ya majukumu mapya, pamoja na ruzuku ya dola 500 (takriban shilingi 500,000/-) kwa kila shule (ukurasa 13).

- *Kuimarisha usimamizi wa fedha*: Usimamizi wa fedha utaimarishwa kuanzia ngazi ya taifa hadi shule, hususan uwajibikaji wa matumizi ya ruzuku ya uendeshaji, ya maendeleo na ya uwezeshaji. Lengo kubwa ni kujenga uwezo wa kutayarisha taratibu, vitabu vya mahesabu na mafunzo kwa kuwezesha kuorodhesha, kuripoti na kukagua matumizi ya fedha za MMEM. Kanuni ya "uwajibikaji na uwazi juu ya matumizi ya fedha za umma itasisitizwa"' na taarifa juu ya matumizi ya fedha za MMEM "zitatolewa kwa ngazi zote za mfumo wa elimu, wakiwemo wazazi na jumuiya" (ukurasa 14).

- *Kuboresha usimamizi wa taarifa za elimu:* Usimamizi wa taarifa za elimu (EMIS) utaangaliwa upya na wasimamizi kupewa mafunzo, kuhakikisha wanawasilisha taarifa sahihi kwa wadau wote kwa wakati (ukurasa 14).

4. Muundo wa Taasisi

Sehemu ya nne ya MMEM ni kujenga uwezo wa taasisi katika mfumo wote wa elimu, kwa kuwezesha demokrasia, mgawanyo wa madaraka, uwajibikaji, ushiriki mkubwa wa umma na kutoa madaraka ya usimamizi wa fedha kwa shule. Hii itaendana na kuongeza ruzuku kwa ngazi ya shule. Jambo la msingi ni kuhakikisha taarifa kuhusu MMEM zinawafikia kwa wakati wadau wote wakiwemo wanafunzi, wazazi, walimu, na wasimamizi wa elimu nchi nzima. Kiambatanisho cha Uimarishaji wa Taasisi (URT 2001b) kimeeleza kwa ufasaha yote kuhusu MMEM. Kinaelezea wajibu wa kila wizara na mamlaka za Serikali za Mitaa, kama halmashauri, ngazi ya kata na kamati za shule. Mambo yaliyotiliwa mkazo katika muundo wa taasisi ni haya yafuatayo:

- *Kamati ya kuratibu*: Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP) ni kamati inayoongozwa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu ina jukumu la kuratibu MMEM. Katika ngazi hii Kamati Maendeleo ya Elimu ya Msingi (BEDC) itasimamia maendeleo ya programu za elimu, mipango na kukagua mipango yote sambamba na sera za Serikali (ukurasa 20). Kamati ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi ina uwakilishi mpana, unaojumuisha wajumbe kutoka serikali, mashirika ya hiari na yasiyo ya serikali, chama cha walimu na wafadhili.

  Ofisi ya Rais -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI*)* ina jukumu la kuhakikisha utoaji wa uhakika wa elimu ya msingi unaofanywa na mamlaka za Serikali za Mitaa, kutoa uongozi wa kimkakati na kujenga uwezo sambamba na kanuni za uboreshaji wa Serikali za Mitaa. Kazi ya Wizara ya Elimu na Utamaduni ni kuandaa mipango shirikishi, kutoa sera na kanuni na kuweka uthibitisho wa viwango bora. Wizara zote mbili zina majukumu ya kutathmini, kukusanya na kusambaza taarifa kwa wadau wote.

- *Kamati za shule*: Kamati za shule ni kiungo muhimu sana katika mfumo wa MMEM. Kisheria kila shule inatakiwa kuwa na kamati ya shule. Kazi zake kuu ni uandaaji wa mipango, bajeti na utekelezaji wa miradi katika njia inayowashirikisha wanafunzi, wazazi, watumishi na wadau wengine. Pia kamati ina uwezo wa kukadiria matumizi ya ruzuku ya maendeleo na uwezeshaji pamoja na kufuatilia matumizi yake na kutoa taarifa. Kamati inatakiwa kufanya shughuli zake kidemokrasia kwa kujali maslahi ya umma. Ushiriki wa jumuiya na uwajibikaji ni muhimu na uonekane kupitia wanaounda kamati za shule.

- *Halmashauri za Wanafunzi na Mabaraza ya Shule*: Chini ya MMEM wanafunzi wana nafasi muhimu katika usimamizi wa shule, katika utekelezaji wa MMEM. Halmashauri ya wanafunzi itakayokuwa na wajumbe wawili kuanzia darasa la 3 - 7 (na 2 hadi 4 kutoka vikundi maalum kama wanafunzi wenye ulemavu), itakutana mara moja kila mwezi kuongelea maslahi ya wanafunzi. Kutoka halmashauri yao wanafunzi wawili (wakike na wakiume) watachaguliwa kidemokrasia na wenzao kuwawakilisha katika kamati ya shule. Mwalimu atahudhuria mkutano wa Baraza la wanafunzi kama mwangalizi tu, kuwezesha kuendeleza uwezo na kupeana taarifa. Anapaswa kuepuka kutawala mkutano (kiambatanisho 6).

- *Ngazi ya Kijiji/Mtaa:* Kazi kubwa ya halmashauri ya Kijiji/Mtaa ni pamoja na uangalizi wa jumla wa kamati ya shule na kuhimiza utoaji wa taarifa za elimu kwa umma. Vile vile kuhimiza wazazi na walezi kuwaandikisha watoto na kutoa michango ya hiari, na

kuzishirikisha asasi zisizo za serikali (AZISE) na mashirika ya jumuiya kutoa ushirikiano katika MMEM

- *Ngazi ya Kata:* Kata ndiyo kiungo muhimu kati ya shule/jumuiya na ngazi ya wilaya. Kamati ya maendeleo ya kata ndiyo yenye jukumu la kuangalia utekelezaji wa shughuli zote za MMEM katika kata, pamoja na kuhamasisha AZISE na mashirika ya jumuiya kuiunga mkono. Mratibu wa elimu wa kata anatakiwa kuhakikisha watoto wote waliofikia umri wa kwenda shule wanaandikishwa na kutoa taarifa za elimu kwa wadau wote katika kata. Pia anatakiwa kusaidia kutambua maeneo muhimu kwa maendeleo ya shule.

- *Mamlaka za Serikali za Mitaa:* Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambazo ni pamoja na Afisa Elimu wa Wilaya, zina jukumu la kusimamia utekelezaji wa mipango yote katika ngazi ya wilaya. Chini ya MMEM, serikali za mitaa zitajitoa katika shughuli za kiutendaji moja kwa moja na badala yake kutoa msaada wa kitaalamu na mipangilio kwa kamati za shule na halmashauri za vijiji. Kazi zao ni kutayarisha mipango ya maendeleo shirikishi, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa MMEM, kusambaza fedha na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa kamati za shule na kuwasilisha taarifa muhimu kwa wadau. Mamlaka za serikali za mitaa zinatakiwa kushirikisha AZISE na mashirika ya jumuiya katika shughuli hii.

- *Wafadhili na AZISE*: MMEM inatoa nafasi kwa ushiriki wa wafadhili na AZISE katika masuala ya elimu nchini. Mtindo uliokuwepo wa kila mfadhili kuchagua mradi wake na kusababisha mgawanyiko unapaswa kuachwa. Wafadhili wanatakiwa kuongeza nguvu katika kuendeleza mipango ya Serikali na mifumo yake. Misaada ya wafadhili itaunganishwa katika bajeti ya Serikali au makusanyo mengine ya ufadhili na mapitio ya matumizi ya umma.

Serikali inaridhishwa na ushiriki mashirika ya hiari zikiwemo Azise na mashirika ya kijamii. Kazi yao kubwa ni kushiriki kikamilifu katika kupanga mipango, utekelezaji, ufuatiliaji na kukagua mipango ya utoaji elimu katika ngazi zote. AZISE zinatakiwa kuchangia utaalamu, ujuzi na rasilimali kuboresha elimu ya msingi, na kushughulika na uchambuzi wa sera na utetezi. Wawakilishi wa AZISE na wafadhili ni wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (BEDC).

Bajeti

Mgao kwa elimu ya msingi hauna budi kuongezwa kwa kiwango cha kuridhisha, kujumuisha malengo ya MMEM ya upatikanaji, kujenga uwezo na majukumu ya kiutawala. Matumizi makubwa yakiwa mishahara ya walimu, mafunzo kwa walimu, na ruzuku ya uendeshaji, maendeleo na kujenga uwezo.

Jumla ya mkadirio wa bajeti wa MMEM (kwa mabilioni ya shilingi) kwa kiwango cha 2001/2 (ukurasa 3) ni:

2002	**2003**	**2004**	**2005**	**2006**	**Jumla (miaka 5)**
299.5	323.0	364.4	344.6	356.4	1,687.9

Gharama halisi bado kuainishwa kwa mpango mzima wa MMEM na inaweza kupelekea tarakimu hizi kubadilika. Serikali ipo tayari kuwekeza asilimia 25 ya matumizi yake ya kawaida kwa sekta ya elimu. Kati ya hizi asilimia 62 itapelekwa kwenye elimu ya msingi. Makusanyo mazuri ya kodi yamaanishe rasilimali zaidi inawekezwa kwenye elimu.

Licha ya haya pengo kubwa kifedha linatarajiwa kati ya rasilimali iliyopo na ile inayohitajika. Serikali itafanya majadiliano kupata msaada mkubwa zaidi wa kifedha kutoka kwa wafadhili

kufidia mapungufu ya bajeti. Hii ni kutokana na ahadi ya mashirika ya kimataifa na nchi matajiri katika mkutano wa Dakar wa 2000 ulioazimia “kuwa hakuna nchi yenye mpango mzuri wa kuendeleza elimu itashindwa kufanya hivyo, kutokana na upungufu wa rasilimali”.

Marejeo

United Republic of Tanzania – URT (2001a) Primary Education Development Plan 2002-2006 (PEDP), Dar es Salaam

URT (2001b) PEDP Strengtherning Institutional Arrangements Annex, Dar es Salaam

URT (2000) Poverty Reduction Strategy, Dar es Salaam

URT (1998) Policy Paper on Local Government Reform, President’s Office Regional Administration and Local Government, Dar es Salaam